MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.08. Msimu wa Kilimo 2023/24* *Tathmini ya Disemba 11-20, 2023 na Matazamio kwa Kipindi cha Disemba 21-31, 2023*

## MUHTASARI

- Hali ya mazao na malisho katika maeneo mengi nchini ni nzuri.
- Mvua zinazotarajiwa katika maeneo machache zitasaidia uoteshaji mbegu na ukuaji wa mazao.
- Wakulima na wafugaji wanashauriwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu hali ya mazao na mashamba ili kuweza kukabiliana na athari mbalimbali zinazoweza kujitokeza


## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 11-20, 2023

Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kupungua nguvu wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika. Hali hii iliendelea kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kuwepo katika maeneo ya nchi.

Joto la bahari la juu kidogo ya wastani liliendelea kuwepo katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi wakati joto la bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani liliendelea kuwepo katika eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi. Hali hii ilichangia kusababisha upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani nchini.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 11-20, 2023

Maeneo mengi nchini yalipata mvua kati ya milimita (mm) 10 hadi 150 na baadhi ya maeneo yaliyo salia yalipata mvua chini ya mm 10 hususan katika mkoa wa Ruvuma, Njombe, kusini mwa Morogoro na Dodoma. Angalia Kielelezo 1.




Kielelezo 1: Kiasi cha mvua kwa siku 10 kwa kipindi cha Disemba 11-20, 2023

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 11-20, 2023

Katika dikadi hii, mvua zilizonyesha katika maeneo mengi nchini zilisaidia ukuaji na maendeleo ya mazao.

Maeneo yanayopata mvua za vuli hususan pwani ya kaskazini, nyanda za juu kaskazini na maeneo yanayozunguka Ziwa Victoria mahindi yapo katika hatua mbalimbali za ukuaji, isipokuwa katika mkoa wa Kagera ambapo mahindi yaliyopandwa mapema yapo katika hatua ya kukomaa na kwa mkoa wa Tanga yapo katika hatua ya kutoa mbelewele.

Mahindi katika maeneo yanayopata mvua za Msimu yapo katika hatua ya kuota na jani la tatu na wakulima wachache waliendelea na shughuli za upandaji.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyama umeendelea kuimarika nchini.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 11-20, 2023

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mabonde vimeongezeka kutokana na mvua zinazoendelea.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 21-31, 2023

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kupungua nguvu kidogo wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuimarika kidogo. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kusogea kidogo kuelekea kusini na kuwepo katika baadhi ya maeneo nchini.

Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la magharibi mwa baharí ya Hindi wakati joto la bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani linatarajiwa kuwepo katika eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 21-31, 2023

Maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kuwa na mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache

Mikoa ya magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kuwa na mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani, na Dar es Salaam vikiwemo visiwa vya Unguja na Pemba) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro) inatarajiwa vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) pamoja na pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) zinatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) na kanda ya kati yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua katika maeneo machache.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) na yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua katika maeneo machache hususan katika nusu ya kwanza ya dekadi.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 21-31, 2023

Mvua zinazotarajiwa katika maeneo machache zitasaidia uoteshaji mbegu na ukuaji wa mazao.

Wakulima wanashauriwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu hali ya mazao ili kuweza kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na unyevunyevu wa udongo wa kupitiliza, kutuama kwa maji kwa mashamba yaliyoko mabondeni, na milipuko ya wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea pale vitakapojitokeza. Aidha, ukaushaji wa mazao, palizi na matumizi ya pembejeo vinatarajiwa kuathirika kutokana na vipindi vingi vya mvua na unyevu wa kupitiliza.

Wavuvi wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya ufugaji wa samaki, na kuchukua tahadhari kwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, hususan kwenye bahari ya Hindi na Maziwa Makuu ili kufanya maamuzi juu ya wakati sahihi wa kwenda kufanya shughuli za uvuvi ili kuepuka athari zitokanazo na upepo mkali na mvua kubwa pale vinapojitokeza.

Wafugaji wanashauriwa kupanda majani ya kutosha na kuchimba mabwawa ya kuvuna maji ya mvua kwakwa matumizi ya baadae.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA DISEMBA 21-31, 2023

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kuongezeka kutokana na mvua zinayoendelea. Jamii inashauriwa kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya baadaye.